KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

# Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 20, Issue 2
16th Rabi uth-Thaani 1433
9th Mar, 2012

# SWALA YA JAMAA YA PILI KWENYE MSIKITI MMOJA

**Na: Sheikh Muhammad Naasir ud-Deen al-Albaani**

**Suali:** Jee, ni nini hukmu ya Kisheria kuhusu kuunga swala ya jama'ah ya pili kwenye msikiti mmoja?

**Jawabu:** Wanavyuoni wa Fiqh wamekhitalifiana kuhusu hukmu ya kuunga swala ya jama'ah ya pili. Hata hivyo, kabla ya kuzitaja ikhtilafu hizo na kuibainisha iliyo ya sawa, itatulazimu kwanza kuitambua hiyo aina ya jama'ah ambayo wanayokhitalifiana kwayo.

Jambo la ugomvi linahusiana na jama'ah inayotekelezwa kwenye msikiti wenye *Imaam na muadh-dhin* walioajiriwa na wenye kudumu. Ama kuhusu jama'ah zinazotekelezwa mahali pengine popote, ikiwa ni nyumbani kwa mtu, msikiti uliojengwa barabarani (k.m Musalla) au kwenye ghala, basi hapana kizuizi chochote cha kumzuia mtu kutoswali jama'ah nyengine kwenye sehemu hizo.

Wanavyuoni wenye kushikilia rai yakwamba ni jambo lenye kuchukiza kuwa na jama'ah nyingi katika misikiti iliyokwishatajwa hapo juu, ile ambayo yenye Imaam na muadh-dhin wa kudumu, hukmu yao imetokamana na ushuhuda kutoka kwenye njia mbili. Ushuhuda wa kwanza ni vifungu vya maandishi kutoka kwa Hakimu Alietukuka. Ushuhuda mwengine ni makisio ya ki-akili ambayo ni kuzitafakari riwaya na hikma zilizosababisha swala za jama'ah. Ama kuhusu ushuhuda wa maandishi, basi wao wamechunguza na kuona yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika uhai wake alikuwa akiwaongoza watu kwenye swala za jama'ah katika msikiti wake. Walaakin, ilipokuwa yeyote miongoni mwa maswahaba zake wanapoingia msikitini na kuona yakwamba swala ya jama'ah imekwisha, wao huswali kila mmoja peke yake bila ya kungojea (wengine waje).Wala hageuki kuliani wala kushotoni kama wanavyofanya watu leo, wakimtafuta mtu mmoja au watu wengi ili aswali nao kama Imaam wao.

Hawakuwa wakifanya hivi Ma-Salaf. Kwahivyo mmoja wao aingiapo msikitini na kuona yakwamba watu wameshaswali, yeye huswali peke yake. Hivi ndivyo alivyokatikiwa Imaam ash-Shaafi' katika kitabu chake kiitwacho AL-UMM, na huja yake katika mas-ala haya ni miongoni mwa mazungumzo yenye kufahamika mno katika mazungumzo niliyowahi kuyaona kutoka kwa majadiliano ya ma-Imaam hata akasema: "Iwapo kipote cha watu wameingia msikitini na wakaona yakwamba Imaam ameshamaliza kuswali, basi nao nawaswali kila mmoja peke yake. Lakini ikiwa wataswali jama'ah, basi swala yao ni yenye kukubaliwa na inasihi, hata hivyo kitendo chao hicho kinanichukiza mimi kwani hiyo si katika desturi ya Ma-Salaf."

Akaendelea kusema: "Amma kuhusu msikiti ulioko kwenye njia kuu, usio na Imaam na muadh-dhin walioajiriwa na wenye kudumu basi hapana madhara yoyote ya kufanya idadi nyingi ya swala za jama'ah hapo. Kisha akasema: "Tumehifadhi sisi yakwamba kipote cha maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) walikosa swala za jama'ah nao wakaswali kila mmoja peke yake. Hata kama walikuwa na uwezo wa kujumuika na kuswali pamoja kwa mara ya pili, hawakufanya hivyo kwa sababu walichukia kufanya (tena) swala ya jama'ah kwenye msikiti mara ya pili."

Huu ni msemo wa Imaam ash-shaafi'. Na alipotaja habari za maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakuwa walikuwa wakiswali kila mmoja peke yake walipokuwa wakikosa swala za jama'ah, zimetajwa habari hizi kwa njia ya riwaya *ta'leeq* kwa ufupi. Nae al-Haafidh Abu-Bakr Ibn Abee Shaybah akazihamisha hizo kwenye kitabu chake maarufu kiitwacho al-Musannaf. Akaipokea kwa riwaya yenye nguvu kutoka kwa al-Hassan al-Basree yakwamba Maswahaba walipokuwa wakikosa swala ya jama'ah, walikuwa wakiswali kila mmoja peke yake. Ibn al-Qaasim akahadithia muelekeo huu kwenye kitabu chake kiitwacho*Mudawwanaat-ul-Imaam Maalik* kuhusu kipote cha Ma-Salaf, kama Naafi', mfanyi kazi wa Ibn 'Umar, saalim ibn 'Abdillah na wengineo, yakwamba wanapokosa swala, wataswali kila mmoja peke yake na hawatofanya swala ya jama'ah mara ya pili.

Vile-vile ikapokewa kutoka kwa Imaam at-Tabaraanee kutoka katika kitabu chake *Mu'jam al-Kabeer* kwa njia nzuri ya upokezi kutoka kwa Ibn Mas'ood yakwamba siku moja alitoka nyumbani kwake pamoja na maswaahib zake wawili kuelekea msikitini ili wakaswali swala ya jama'ah. Lakini walipofika hapo, waliwaona watu wakitoka msikitini, kwani walikuwa tayari wamemaliza kuswali. Akarudi nyumbani kwake na akawaongoza kwenye swala. Kwahivyo huku kurudi kwa Ibn Mas'ood- Kama alivyo kutokana na mkuruba wake mkubwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) na 'ilmu alokuwa nayo ya kuufahamu Uislamu- ikiwa alikuwa yuwajuwa maamrisho ya kuswali jama'ah nyingi kwenye msikiti mmoja, basi angeliingia na maswaahib zake wawili na akaswali jama'ah pamoja nao. Alifanya hivyo kutokana na kuyaelewa maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema:

"Swala iliyo bora ya mtu ni ile anayoiswali nyumbani kwake, isipokuwa kwa swala ya faradhi." Sasa ni kitu gani kilichomzuia Ibn Mas'ood (رضي الله عنه) asiswali swala hii ya faradhi msikitini?- kufahamu kwake

**YALIYOMO**

JAMAA YA PILI 1 - 3
3 - 4

iwapo angeliswali msikitini ingelimbidi aiswali peke yake. Kwahivyo akaona yakwamba ingelikuwa ni bora akaswali nao jama'ah nyumbani kwake kuliko wangeliswali kila mmoja peke yake msikitini. Kwa ujumla, hayo ni maelezo yanayokubaliana na maoni ya wanavyuoni wengi wasiopendekeza jama'ah nyingi zinazofanywa kwenye misikiti iliyo kwenye hali zilizotajwa hapo mbeleni.

Baada ya yote hayo, watu hawatokosa kuona kupata ushahidi mwingine pindi watakapochunguza na kufanya upekuzi. Hivyo basi, maimamu wawili, al-Bukhari na Muslim wamepokea kutoka kwa hadeeth ya Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: ***"Natamani kumuamrisha mtu aongoze watu kwenye swala. Kisha niwaamrishe watu watafute kuni za moto, wawafuate wale watu walioacha kuja kuswali jama'ah na wazichome nyumba zao. Naapa kwa yule ambae Mikono Yake imeimiliki roho ya Muhammad, lau kama mmoja wao angelijua yakwamba akija msikitini atapata wanyama wawili wazuri waliowindwa (hunted), kwahakika angelikuja na kuwashuhudia hao (wanyama) wawili".*** Katika hadeeth hii Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitoa tisho kali kwa wale wanaoepuka kuhudhuria swala za jama'ah msikitini kwa kuwachoma kwa moto. Mimi naamini yakwamba hadeeth hii peke yake inatupasha habari sisi kuhusu hukmu iliyokwisha tajwa hapo mbeleni au inatueleza sisi kuhusu alivyosema Imaam ash-Shaafi' *(رحمه الله)* na alivyoeleza Ibn Abee Shaybah. Nayo ni kwamba maswahaba hawakuwa wakirudia swala ya jama'ah kwenye msikiti. Kwahivyo, ikiwa sisi tutachukulia yakuwa zile jama'ah za ziada (ya pili, tatu...) misikitini zinakubaliwa kisheria, baadae likaja hili tisho kubwa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa wale wenye kuepuka kuhudhuria swala ya jama'ah, ni jama'ah ipi hiyo wanayoiepuka? Na ni kwa jama'ah ipi hiyo waliyoiepuka kuhudhuria lilikusudiwa tisho hili kubwa? Ikiwa mtu atasema: "Ni kwa jama'ah yakwanza", basi ni sharuti ikubalike pia hizi jama'ah nyengine haziruhusiwi kisheria. Na ikiwa mtu atasema: "Onyo hilo kali limemkusudia yule mwenye kuacha kila swala ya jama'ah, hata zikawa ni nyingi kiasi cha kwamba idadi yake ikawa ni yenye kuendelea". Basi katika hali hii, hoja ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) dhidi ya yeyote miongoni mwa walioziepuka jama'ah yoyote haitoweza kuthubutu kabisa. Kwahivyo, kama angelimshangaza mmoja wao, baada ya kumuwakilisha mtu aongoze swala, kwa kumuingilia nyumbani kwake na akamuona apitisha wakati kwa kustarehe na mkewe na watoto. Basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) amgombeze kwa hilo na kumwambia: "Kwanini huendi kuswali na jama'ah? Atamjibu kwa urahisi: "Mimi nitaswali na jama'ah ya pili au ya tatu". Sasa jee, hoja ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) inaweza kuthibitishwa dhidi ya mtu huyu? Kwa ajili hii, matamanio makubwa ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) ya kumuamrisha mtu amuwakilishe kwenye kuwaswalisha watu ili yeye (صلى الله عليه وسلم) awaendee kwa ghafula wale walioepuka kuhudhuria swala za jama'ah na kuzichomelea mbali nyumba zao, ni ushahidi mkubwa sana yakwamba hapana jama'ah ya pili kabisa. Haya ni kulingana na riwaya za vifungu vya maandishi ambavyo wanavyuoni wamevitegemea kwa kutolea ushahidi wao.

Ama kuhusu uchunguzi, basi ni kutoka kwenye pembe ifuatayo: Zimepokewa Ahaadeeth nyingi zenye kutaja fadhila za swala za jama'ah. Miongoni mwa hadeeth hizo ni pale aliposema (صلى الله عليه وسلم): ***"Swala ya jama'ah ni bora kuliko swala ya mtu peke yake kwa daraja ishirini na tano"***- na kwenye riwaya nyengine ***"ishirini na saba"***. Kwahivyo, fadhila iliyo bora imetajwa kwa swala ya jama'ah peke yake.

Na vilevile ikatajwa kwenye hadeeth nyengine: ***"Swala ya watu wawili mbele ya Allaah ni bora kuliko swala ya mtu peke yake. Na swala ya mtu pamoja na watu wawili wengine ni bora mbele ya Allaah kuliko swala yake na mtu mmoja".***

Hii ni kwa sababu kila jama'ah inapo-ongezeka idadi ya watu malipo yake yanazidi mbele ya Allaah. Kwahivyo, tukiwa na fahamu hii kwenye akili zetu na tukiangalia mambo yaliosababishwa na rai zenye kuruhusu jama'ah za ziada kwenye msikiti wenye Imaam wa kudumu, basi matokeo yake si yenye kuridhisha. Hii ni kwa sababu rai ya kufanya jama'ah zenye kurudiwa mara kwa mara husababisha kupunguza idadi ya watu wenye kuhudhuria jama'ah ya kwanza. Na hivi ni kwenda kinyume na hima inayopatikana kwenye hadeeth: ***"Swala ya mtu mmoja akiwa na mwenziwe ni bora kuliko ya mtu mmoja peke yake",*** kwani hadeeth hii inatuhimiza watu wengi kwenye jama'ah. Na kuishikilia rai yakwamba jama'ah inaweza kurudiwa kwenye msikiti, kutokana na dharura, inasababisha upungufu wa idadi ya watu katika jama'ah yakwanza iliyoshurutishwa kisheria na mgawanyiko wa umoja wa waislamu.

Na pana jambo jengine la mazingatio. Ni lazima tukumbuke yakwamba hadeeth ya Ibn Mas'ood (رضي الله عنه) katika Saheeh Muslim kama vile hadeeth ya Abu Hurairah (رضي الله عنه): ***"Natamani kumuamrisha mtu aongoze watu kwenye swala".*** Matamshi haya yalikusudiwa wale walioacha kwenda kuswali swala ya Ijumaa. Hivyobasi, tunapojua sisi, Ibn Mas'ood (رضي الله عنه) ametoa onyo kali la kuhusu jambo fulani juu ya kila anaeacha swala ya Jama'ah, basi tunafahamu yakwamba makusudio hapa ni Jama'ah. Kwa hakika, maana ya maonyo haya ni kwamba haifai kuwepo jama'ah ya pili baada ya aina hizi mbili za swala. Ndio utaona, swala ya Ijumaa-mpaka hivi leo imehifadhiwa upweke wake na wala haipatikani rai isemayo kuwa yafaa kuwepo swala nyingi za Ijumaa katika msikiti mmoja. Wanavyuoni wote, juu ya tofauti zao, wanakubaliana kuhusu jambo hilo. Kwa ajili hii, ndio tunaona misikiti inafurika watu ifikapo siku ya Ijumaa. Tusighafilike bali pia tukumbuke yakwamba miongoni mwa sababu za misikiti kujaa siku za Ijumaa ni kwamba wanahudhuria hapo wale wasioswali swala yoyote nyengine isipokuwa Ijumaa. Hata hivyo, bila ya shaka yoyote sababu ya misikiti kujaa watu siku ya Ijumaa ni kwamba Waislamu- na sifa zote ni zenye kumthubutukia Allaah-hawaswali swala ya Ijumaa kwa mara ya pili (mfululizo) kwenye msikiti uliokwisha swaliwa. Kwahivyo, ingelikuwa Waislamu wanazitekeleza swala za Jama'ah kama vile wanavyotekeleza swala za Ijumaa na kama yalivyokuwa mambo hayo yakitekelezwa wakati wa Mtume (صلى الله عليه وسلم), basi misikiti ingelijaa watu. Angeliwajibika kila mwenye kuswali swala ya Ijumaa pasi na kukosa kufahamu yakwamba iwapo ataikosa Jama'ah ya kwanza, hatopata badala yake. Na Imani hii ndio itakuwa chombo cha kumuhimizia na kumfanya akumbuke kuhudhuria swala za Jama'ah. Na kinyume cha hivyo pia ni jambo linalowezekana muislamu akiwa na imani yakwamba iwapo yeye atakosa Jama'ah ya kwanza, basi hapana shaka yakwamba atapata Jama'ah ya pili, au ya tatu au wakati mwengine hata ya kumi. Basi haya ni miongoni mwa mambo yatakayo kuzidho-ofisha

jitihada zake na bidii asiweze kuhudhuria Jama'ah ya kwanza. Kuna mambo mawili yaliotukabili sisi:

**JAMBO LA KWANZA:**

Ni lazima tubainishe yakwamba wale walio na rai yakwamba Jama'ah ya pili, kulingana na masharti tulokwisha yaeleza hapo mbeleni, si katika kanuni za kisheria na ni wale ambao waliosema jambo hilo ni la kuchukiza, nao ni idadi kubwa ya Ma-Salaf. Miongoni mwao wakiwemo maimamu watatu- Abu Haneefah, Maalik, na ash -Shaafi'. Kulingana na riwaya moja, imethubutu yakwamba Imaam Ahmad ni miongoni mwao. Riwaya hiyo hata hivyo, si mashuhuri sana miongoni mwa wafuasi wake ingawa mmoja wa wanafunzi wake, Abu Daawud as-Sijistaanee amewahi kuitaja. Akahadithia kutoka kwake katika kitabu chake *Masaail al-Imaam Ahmad* yakwamba (Ahmad) amesema:*"Kurudia swala ya Jama'ah katika misikiti miwili mitukufu (K.M Makkah na Madeenah) kunaleta daraja kubwa sana ya kutoridhia (kiraaha)"*.Kwahivyo katika hali ya mapendekezo vilevile tunapata ishara fulani ya makatazo ya kuregelea Jama'ah kwenye misikiti mengine. Walaakin hali hiyo ya makatazo imetiliwa mkazo kwenye misikiti (mitukufu) miwili. Basi kulingana na riwaya hii, Imaam Ahmad yu-katika msururu wa ma-Imaam wengine watatu kwenye msimamo huo.

**JAMBO LA PILI:**

Riwaya nyengine ya Imaam Ahmad- ile iliyo mashuhuri mno kwa wanafunzi wake-yeye (رحمه الله) na wale wafasiri waliomfuata wameijengea huja kutokana na hadeeth iliyopokewa na at-Tirmidhee, Imaam Ahmad na wengineo. Nayo ni hadeeth ya Abu Sa'eed al-Khudhree (رضي الله عنه) pindi aliposema:*"Mtu fulani aliingia msikitini wakati Mtume* (صلى الله عليه وسلم) *alipokuwa amesha-maliza kuswalisha na maswahaba zake wamemzingira. Mtu huyu alikuwa akitaka kuswali, kwahivyo akasema Mtume* ( صلى الله عليه وسلم)*: **'Hapana mtu awezae kumpa sadaka mtu huyu kwa kuswali nae?',** basi akasimama mtu mmoja na akaswali nae."*

Na kwenye riwaya ya Abu Bakr al-Baihaqee, ipatikanayo kwenye kitabu chake cha *Sunan al-Kubraa*, imeelezwa hapo yakuwa mtu huyu alikuwa ni Abu Bakr as-Siddeeq. Lakini, riwaya hii ina illa kwenye upokezi wake. Riwaya iliyo saheeh haikumtaja mtu kwa jina. Basi (Wanavyuoni) hawa wameitumia hadeeth hii kama ni ushahidi na kusema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) ameliruhusu jambo la kuwepo kwa Jama'ah ya pili!"

**MAKUSUDIO YA HADEETH HIYO:**

Kwa kuwajibu wenye kuutumia ushahidi huu, inatupasa kuizingatia Jama'ah iliyokusudiwa na hadeeth hii kuwa hailingani na Jama'ah iliyo-ashiriwa kwenye suala. Kwa sababu Jama'ah iliyokusudiwa na hadeeth hii ni Jama'ah ya mtu alieingia msikitini baada ya kumalizika Jama'ah ya kwanza na akakusudia kuswali peke yake. Lakini "Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawahimiza maswahaba zake ambao tayari wameshaswali nae, ainuke mmoja wao kwa kujitolea ili aswali swala ya nawaafil. Mmoja akajitokeza na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Sasa Jama'ah hii ilikuwa ni ya watu wawili. Aongozae swala hiyo (Imaam) na aongozwae (Ma'moom). Imaam akaswali swala yake ya faradhi na Ma'moom akaswali swala ya Nawaafil. Sasa ni nani hapa aunganishae Jama'ah hii? Ingelikuwa si yule mwenye kuswali swala ya nawaafil, basi hapangelikuwa na Jama'ah. Kwahivyo hiyo ni Jama'ah ya faradhi na nawaafil, na wala sio Jama'ah ya faradhi. Na huku kutafautiana (Kulikotajwa kwenye Suala) ni kuhusiana na Jama'ah ya pili ya swala ya faradhi. Kwahivyo kutokana na haya, kuitumia hadeeth ya Abu Sa'eed al-Khudhree kama ushahidi katika mabishano haya ni makosa. Hapana shaka jambo lenye kuthibitisha ukweli zaidi ni hadeeth isemayo:***"Hapana mtu awezae kumpa sadaqah mtu huyu kwa kuswali nae?*** Katika tukio hili, palikuwa na mtu atoae sadaqah na mwengine apokeae. Sasa ikiwa tutamuuliza mtu sisi mwenye chembechembe za ili na ufahamu: "Ni nani hapa atoae sadaqah na ni nani apokeae katika hali hii, ambayo Mtume ( صلى الله عليه وسلم) ameiridhia?". Jawabu itakuwa: "Mwenye kutoa sadaqah ni yule mwenye kuswali nawaafil ambae aliekwisha kuswali swala ya faradhi nyuma ya Mtume wa Allaah ( صلى الله عليه وسلم), na yule anaepokea sadaqah ni yule aliekuja msikitini kuchelewa."

Sasa tukilivurumiza Suala hili kwa jama'ah iliyo na mizozo hivi sasa. Kwa mfano watu sita ama saba wakiingia msikitini na wakaona yakwamba Imaam ashamaliza kuswalisha. Mmoja wao akaongoza swala na wengine wakamfuata kwenye jama'ah ya pili. Ni yupi miongoni mwao atoae Sadaqah hapa? Na ni yupi apokeae sadaqah? Hakuna yeyote atakaetoa jawabu iliyo sawa kama ilivyo kwenye mfano wa kwanza. Jama'ah hii (ya watu) walioingia msikitini baada ya Imaam kumaliza kuswalisha, wote hawa wanaswali swala ya faradhi. Hapana yeyote atoae sadaqah, wala hapana yeyote apokeae sadaqah. Kinyume chake, giza hili limebaini na kudhihiri kwenye mfano wa kwanza.

Anaetoa sadaqah ni yule anaeswali swala ya nawaafil ambae amesha-swali nyuma ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). Swala yake imehifadhiwa kwa daraja ishirini na saba (za ujira). Kwa ajili hiyo, yeye ni tajiri kwahivyo ana uwezo wa kutoa sadaqah kwa wengine. Na mwenye kuongoza swala- lau isingelikuwa ni kwa ajili ya yule atoae sadaqah, basi angeliswali peke yake- yeye ni masikini na anahitaji mtu ampe sadaqah. Kwani yeye hakupata kile alichokipata yule anaempa yeye sadaqah (katika thawabu)

Sababu za huyu mtu kuwa yeye ndie atoae sadaqah na yule mwengine kuwa ni mpokezi wa sadaqah ni wazi. Ama kuhusu hali ya mzozo tulionayo hivi sasa basi hali hii yahitaji kubainishwa, kwani wanaoswali wote ni masikini kwa sababu wote wamezikosa fadhila za Jama'ah ya kwanza. Kwa hivyo, maneno ya Mtume ( صلى الله عليه وسلم)*:**"Hapana mtu awezae kumpa sadaqah mtu huyu kwa kuswali nae?"*** hayatumiki hapa. Hivyo basi, kwenye hali kama hii, haifai kutumia tukio hili (lilotajwa kwenye Hadeeth) kama ushahidi. Wala haiwezi kutumiwa kama kumbukumbu ya mas-ala haya ambayo ndiyo majadiliano yetu. Tutayaunganisha mas-ala haya na ushahidi mwengine wanaoutumia kama dalili zao ambazo ni maneno ya Mtume ( صلى الله عليه وسلم):***"Kuswali na Jama'ah ni bora zaidi kuliko kuswali peke yako kwa daraja ishirini na saba "*** Kwahivyo hapa wanatumia makusudio ya ki-ujumla (kwenye hadeeth) kama ushahidi, kwa maana ya kwamba wamelifahamu tamshi **"Fee"** kabla ya tamshi la Jama'ah ni lenye makusudio yenye kuhusisha (Jama'ah zote). Ikiwa na maana (kulingana na wanavyofahamu wao) ya kila Jama'ah ni bora zaidi kuliko kuswali peke yako. Tunajibu kwa kusema, kulingana na ushahidi tulokwisha utaja yakwamba tamshi hilo la **"Fee"** halikukusudiwa kwa kuhusisha Jama'ah zote, bali linahusu makusudio maalum. Ikiwa na maana ya kwamba, swala ya Jama'ah- iliyofunzwa na Mtume ( صلى الله عليه وسلم), ikahimizwa watu na kuamrishwa kuihudhuria, wakatishwa wenye kuipuuza kwa kuchomwa nyumba zao na wale wenye kuipuuza wakajulikana kama wanafiki- ndiyo swala

ya Jama'ah iliyo bora zaidi kuliko kuswali mtu peke yake. Nayo ni swala ya Jama'ah ya kwanza. Na Allaah Mtukufu ndie Mjuzi wa Yote.

## KUJITAYARISHA KWA MAPAMBANO NA MAADUI WA ALLAAH

SUALI: Hapana shaka yoyote yakwamba maadui wa Umma wa Kiislamu wanaotea nafasi muafaka ili wapate kuwatenza nguvu na kuwatawala (Waislamu). Sasa ni njia gani ambazo jambo hilo linaweza kuzuiwa?

JAWABU: Ni wajibu wa Mataifa ya Kiislamu kujiandaa kwa mapambano na maadui wa Allaah na kutahadharisha na kuzifichua njama zao, na kushikamana na Dini ya Allaah na kuwa mashujaa mbele ya haki pamoja na daima kufahamu yakwamba kuna ahadi (ya Allaah kwa waumini), na musiwe ni wenye kudharau wala kuishi kwa amani na njama za maadui, kama alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa): "Enyi mlioamini! Shikeni hadhari yenu (juu ya maadui zenu. Msikhadaike)... " [Soorah an-Nisaa., Aayah 71]. Na pia Akasema (سبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa): "Basi waandalieni (wawekeeni tayari) nguvu mziwezao (vifaru, ndege za kivita, makombora, mizinga, n.k), na mafarasi yaliyofungwa (kufuga), tayari tayari (mipakani), ili kwazo (nguvu hizi) muogopeshe maadui wa Allaah na maadui zenu, (mnaowajua) na pia (maadui zenu) wengineo wasiokuwa wao, msiowajua nyinyi (lakini) Allaah Anawajua. " [Soorah al-Anfaal, Aayah 60]. Kwahivyo, jambo lililowajibu juu ya Mataifa ya Kiislamu, Waarabu na wasiokuwa Waarabu, ni kuitafakari ahadi (ya Allaah kwa Waumini) na kuwa na msimamo juu ya Dini ya Allaah na Sheria Alizotuletea. Na njia bora zaidi za kutafakari ni kuwa na msimamo mzuri juu ya haki na kuwa thabiti juu ya njia hiyo, na kujitegemeza kwa Allaah na Mtume Wake katika nyanja zote, na kuhukumiana kwa Sheria Zake. Hili ni jambo la mazingatio makubwa (ya kiroho). Kisha kuna vifaa na nguvu zinazohitaji kuzingatiwa, (ambayo ni matayarisho) jeshi imara, na (kujipatia) silaha zinazofaa katika wakati huo kadiri ya nguvu zao na uwezo walonao kama ambavyo Allaah Alivyowaamrisha kuyatekeleza yale waliyo na uwezo nayo (peke yake) bila ya kujikalifisha, pindi Aliposema (kama ilivyofasiriwa): "Basi waandalieni nguvu mziwezao tayari tayari..." [al-Anffal, Aayah 60]. Kwahivyo (Mataifa) yote ya Kiislamu yafanye bidii ili wajipatie silaha zinazofaa wakati unapowadia, na wajitahidi kukusudia kutengeza silaha wao wenyewe au (kama hawatoweza) wazinunue. Hapana budi kufanya Jitihada za pamoja ili kujaribu matayarisho ya Jeshi la Kiislamu katika wakati wa utulivu na amani, hata kama zifikapo nyakati za shida, basi (Mataifa ya Kiislamu) nayo yatakuwa na vikosi vya kutosha. Na jambo kubwa lenye umuhimu ni kuirekebisha nafsi yako kwa kumcha Allaah na kuwa na msimamo wa kisawasawa katika Dini Yake, na kujiepusha na madhambi, na kuwa na ikhlaas kwa Allaah katika 'Ibaada, na kukataza kufanya Ibaada za kumshirikisha Allaah (Shirk); kama vile kudumisha ("mawasiliano ya kiroho") na maiti, na kuwaomba usaidizi na kuweka nadhiri kwa kuyatumia majina yao na mifano yake - kwahivyo yote hayo ni kumshirikisha Allaah katika 'Ibaada. Kwahivyo udumishaji wa mawasiliano na waliokufa na kuwaomba wao usaidizi katika mampambano dhidi ya maadui au kuyapoza maradhi, basi yote hayo yanakuwa ni shirk kubwa (yanamfanya mtenda hayo kuwa nje ya mkunjo wa Uislamu). Basi ni wajibu juu ya Mataifa yote (ya Kiislamu) kujitolea huduma zao kwenye suala hili, na kuwaelekeza vijana wao kumpwekesha Allaah katika 'Ibaada (tawheed) kwa ikhlaas, na kujiepusha na kumshirikisha Allaah (سبحانه وتعالى) katika 'Ibaada na kila mmoja awe katika msimamo wa kisawasawa juu ya Dini ya Allaah, na kuwaonya dhidi ya madhambi, na kurudi (kwa kuyatenda matekelezo) kwenye Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) katika nyanja zote za kimaisha, kama ambavyo Alivyosema katika Qur'aan (kulingana na tafsiri): "Enyi mlioamini! Mtiini Allaah na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu, walio katika nyie (Waislamu wenzenu). Na kama mkikhitalifiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Allaah na Mtume, ikiwa mnamwamini Allaah na siku ya mwisho. Hiyo ndiyo kheri, nayo ina matokeo bora kabisa." [an-Nisaa, Aya 59]. Namna hii, Allaah (سبحانه وتعالى) Amewafaridhia Waumini wayafungamanishe mas-ala yote wanayokhitilafiana kwayo na Allaah na Mtume Wake, yaani: wajifungamanishe na Kitabu kitakatifu, ambacho ni Qur'aan, na kwenye Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Sasa kila uongofu utokao katika Kitabu na Sunnah Saheeh, hatuna budi kushikamana nacho, kama alivyosema Allaah ( سبحانه وتعالى) (kulingana na tafsiri): "Na mkikhitalifiana katika jambo lolote (rejeleeni Kitabu cha Allaah na Hadeeth za Mtume kwani) hukumu yake iko kwa Allaah." [Soorah ash-Shooraa, Aayah 10] "...na Allaah ( سبحانه وتعالى) Akawaamrisha washikamane na walee al-amr (kiongozi), katika kila jambo jema; kama alivyosema Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم): (Kwa) Hakika utiifu ni katika (kila) jambo la wema. ...kwahivyo ni wajibu juu ya Mataifa (ya Kiislamu) - baina yao - iwapo kutapatikana kutoelewana, wayarejeze kwa Allaah na Mtume Wake na Hukmu za kisheria, na wakati huohuo wao wenyewe wawe kwenye muelekeo wa kisawasawa katika Dini ya Allaah, na walilekeze Jeshi lao na raia wao kwenye muelekeo huo wa kisawasawa, na hii ndiyo njia inayoelekea katika ushindi, njia ielekeayo katika furaha, na ndiyo njia ielekezayo katika kuheshimika na ubora, na njia ya kujihifadhi dhidi ya maadui popote pale walipo, na jinsi yoyote ile waliyo. Kwahivyo, pindi wao (Mataifa ya Kiislamu) watakapokuwa wamesimama wima (juu ya hii njia ya sawa) na wakasubiri juu ya msimamo huo, basi Allaah Atawatosheleza dhidi ya uovu wa maadui zao na Awape matokeo bora dhidi ya maadui zao, kama Alivyosema (عزّ وجلّ) (kulingana na tafsiri): "Ikikupateni kheri huwasikitisha. Na ikikupateni shari wanaifurahia. Na kama nyinyi mkisubiri na mukawa al-Muttaqoon (mkamcha Mungu) hila zao hazitakudhuruni kitu. Hakika Allaah Anayajua vizuri yote wanayoyatenda." [Soorah Aal-'Imraan, Aayah 120]. Na Akasema ( عزّ وجلّ) (kama ilivyofasiriwa): "...na ni wajibu juu Yetu kuwanusuru walioamini." [ar-Room, Aayah 47]. Na Akasema (عزّ وجلّ) (kama ilivyofasiriwa): "Allaah Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa Atawafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia Dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo; basi hao ndio wavunjao amri Zetu." [an-Noor, Aayah 55]. "...na aayaat zenye maana kama hayo ni nyingi. Na namuomba Allaah Awape Waislamu wote ushindi na uongofu, na Azirekebishe hali za viongozi, na Awape usaidizi katika mambo mema, na Awape ufahamu saheeh wa Dini na Azifanye nyoyo zao kuwa thaabit (Aameen).[Majmoo' Fataawa wa Maqaalaat Mutanawwi'ah - Vol. 6, Uk. 211-214, Suali No.5]. **Sh.Ibn Baaz.**